




## Tahadhari ya kutokea kwa mlipuko wa Homa ya Bonde la Ufa Oktoba-Desemba 2015

### Utangulizi

Taarifa za utabiri wa hali ya hewa duniani kote zinaonesha kuwepo kwa mvua kubwa za El Niño katika kipindi cha Oktoba-Desemba 2015. Kulingana na taarifa rasmi za Mamlaka ya Bahari na Hali ya Hewa ya Marekani na Ofisi ya Hali ya Hewa ya Uingereza, El Niño itaathiri maeneo mengi na kusababisha aidha mvua kubwa ama vipindi virefu vya ukame. Taarifa hizo zinaendelea kueleza kuwa El Niño ya mwaka huu itakuwa na madhara makubwa kuliko vipindi vyote tangu hali hiyo ilipoanishwa mwaka 1950.

Mamlaka za Hali ya Hewa za Tanzania na Kenya nazo zimetoa tahadhari ya kuwepo kwa mvua kubwa “juu ya wastani” katika kipindi cha Oktoba - Desemba 2015. Kwa Tanzania mvua juu ya wastani inategemewa kunyesha katika maeneo yote ambayo yana misimu miwili ya mvua kwa mwaka na baadhi ya maeneo yenye msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Mvua hizi zinategemewa kuambatana na mafuriko makubwa (Ramani 1). Mvua hizi kubwa na mafuriko zina uwezekano mkubwa wa kuambatana na milipuko ya magonjwa, na hasa yale yanayoambukizwa na vidudu nyonya kama mbu. Moja ya magonjwa hayo ni Homa ya Bonde la Ufa.




**Ramani 1: Utabiri wa mvua ulitolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**

Homa ya Bonde la Ufa (HBU) ni ugonjwa unaosababishwa na virusi ambavyo huathiri zaidi ng'ombe, mbuzi, kondoo na binadamu. Wanyama, hasa ng'ombe, mbuzi na kondoo huambukizwa

HBU kwa kuumwa na mbu wenye virusi vya ugonjwa huo. Binadamu hupata ugonjwa huo kwa aidha kuumwa na mbu au kula nyama au mazao mengine kama maziwa na damu kutoka kwa wanyama waliambukizwa HBU. Binadamu anaweza pia kuambukizwa na virusi vya HBU anapogusana na mnyama aliyeambukizwa au kugusa mazao ya kutoka mnyama mwenye virusi vya HBU. Mbu wa jamii ya *Aedes* ndiyo chanzo cha awali cha maambukizo ya HBU. Hata, hivyo mbu wengine wa jamii ya *Culex* na *Anopheles* wanaweza kusababisha maambukizo pale ambapo ugonjwa huo umeshatokea. HBU husambaa kutoka eneo moja hadi jingine kupitia mifugo inayohama kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Kwenye mifugo, HBU inajionesha kwa uwepo na matukio mengi ya ng'ombe, kondoo na mbuzi kutupa mimba au/na kuwepo kwa vifo vya wanyama wachanga. Kwa binadamu, HBU inajionesha kwa watu kupata homa za ghafla, mafua, kutokwa na damu katika sehemu za mwili zilizo wazi, kuchanganyikiwa, na kupoteza uwezo wa kuona vizuri. Dalili hizi kwa binadamu zinajitokeza mara nyingi katika maeneo ambayo mifugo imeathiriwa na HBU.

Mlipuko wa kwanza wa HBU Tanzania ulitokea mwaka 1930. Mchanganuo wa takwimu za matukio ya HBU Tanzania unaonesha kuwa milipuko ya ugonjwa huo imetokea tena katika miaka ya 1947, 1957, 1960, 1963, 1968, 1977/78, 1989, 1997/98 and 2006/07 hii ikiwa ni wastani wa miaka 8 kutoka mlipuko mmoja hadi mwingine. Milipuko yote ya HBU iliyopita imetokea kati ya Desemba na Juni. Milipuko hii, hususani ule mkubwa wa 2006/2007 ulisababisha vifo na uliathiri maisha na uchumi wa mtu mmoja mmoja na wa taifa kwa ujumla. Maeneo ya Tanzania yaliyoathirika na milipuko ya HBU iliyopita ni yale yanayopata misimu miwili ya mvua (masika na vuli). Sehemu kubwa ya maeneo haya yako mashariki mwa Bonde la Ufa.




**Ramani 2: Utabiri wa ongezeko la hatari ya kutokea milipuko ya HBU kulingana na mtawanyiko wa mbu jamii ya *Culex* Tanzania hadi mwaka 2020 (kushoto) na mwaka 2050 (kulia)**

Taarifa za kitafiti na zile za hali ya hewa zimedhihirisha kuwa, milipuko ya HBU Tanzania hutanguliwa na miezi miwili ya mvua kubwa (zaidi ya 400 milimita za ujazo), zinazoambatana na ongezeko kubwa la mbu. Uwepo wa mafuriko na maji mengi yaliyotuma unatoa fursa kubwa kwa mbu kuzaliana na kusambaza virusi vya HBU. Mabadiliko ya tabia nchi na mtawanyiko wa mbu unaonesha kuwa maeneo yaliyo katika hatari ya maambukizo ya HBU yanaongezeka (Ramani 2). Tabia ya kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine linachangia kwa kiasi kikubwa kusambaa virusi va HBU nchini, hivyo kuongeza ukubwa wa tatizo. Utabiri wa maeneo yanayopendelewa na mbu wanaoneza HBU unaonesha dhahiri kuwa kanda ya kaskazini-

mashariki, kanda ya kati, na kanda ya Ziwa Viktoria kuwa na maeneo mazuri ya mazalio ya mbu hao, na hivyo kuwa kwenye hatari kubwa ya kupata mlipuko ya HBU (Ramani 3).

### Tishio la mlipuko wa HBU Tanzania

Ni vizuri kukumbushana kuwa sasa ni miaka 8 tangu Tanzania ilipopatwa na mlipuko wa mwisho, na kipindi hiki cha mwaka kinashabihiana na kipindhi hicho cha 2007. Maelezo ya matukio na mtawanyiko wa mbu waambukizao HBU Tanzania; na uwezekano wa kuwepo kwa mvua za El Nino mwishoni wa 2015 ni ishara tosha za tahadhari za kuwepo kwa mlipuko wa HBU nchini (Ramani 3).



**Ramani 3: Maeneo ya uwezekano mdogo, wa kati na mkubwa wa kutokea mlipuko wa HBU Tanzania**

Tamko hili la tahadhari linatolewa ili kujiandaa na matukio ya mlipuko ya HBU inayoweza kuikumba Tanzania katika kipindi cha kuanzia Oktoba 2015.

### Nini Kifanyike?

Kutokana na ushahidi ulielezwa katika taarifa hii, inapendekezwa kuwa TUSISUBIRI hadi mlipuko wa HBU utokee ndiyo tuchukue tahadhari. Madhara ya HBU yanaweza kuwa makubwa sana na kuambatana na changamoto zitakazoathiri maisha ya wananchi wetu. Ni vyema basi mapendekezo yafuatayo yatekelezwe haraka iwezekanavyo:

- Uchunguzi wa uwepo wa viini kinga vya HBU ufanyike na uambatane na utoaji wa chanjo dhidi ya HBU kwa ng'ombe, kondoo na mbuzi kwenye maeneo yote yaliyo katika hatari ya mlipuko.
- Ufuatiliaji wa taarifa za hali ya hewa na uwezekano wa kutokea mafuriko uimarishwe. Taarifa hizi zitumike kutoa viashiria vya mlipuko katika maeneo mbalimbali ya nchi.
- Wizara zenye dhamana ya afya ya binadamu na mifugo ziratibu ufuatiliaji wa matukio ya ugonjwa na maandalizi ya kuzuia na kupambana na mlipuko.
- Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi iongeze kipengele cha matokeo ya uchunguzi wa maambukizi ya HBU kabla ya kutoa kibali kwa wale wanaotaka kusafirisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine.

- Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi iandae utaratibu kwa kuimarisha mfumo wa utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo.
- Kuandaa mkakati wa makusudi wa kuhakikisha viuatilifu vinavyotumika katika kuogesha mifugo vina uwezo wa kuangamiza vidudu nyonya wakiwemo mbu.
- Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya ziandae utaratibu wa kuwaelimisha wananchi kuhusu kuepuka mambukizo ya HBU ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za kuwepo viashiria vya mlipuko wa HBU katika maeneo yao.
- Wananchi wapewe elimu kuhusu umuhimu wa kuhakikisa nyama inakaguliwa na inapikwa na kuiva, na maziwa yanachemshwa kabla ya kutumiwa na binadamu. Watu waepuke kula mizoga na mizoga yote iharibiwe chini ya uangalizi wa maofisa wenye majukumu hayo.
- Jamii za wafugaji waelemishwe kuhusu dalili za HBU katika mifugo na umuhimu wa kutoa taarifa haraka kwenye mamlaka zinazohusikia katika maeneo yao.
- Maabara za Taifa za Afya ya Mifugo na Binadamu zianze kuandaa maabara zao dhidi ya tishio la mlipuko wa HBU ili kuweza kuthibitisha mapema tukio lolote la ugonjwa huo.
- Wito kwa watoa huduma katika vituo vya afya kutilia maanani uwezekano wa kuwepo kwa maambukizi ya HBU kwa wagonjwa wa homa wanaowahudumia.
- Vifaa ya kuzua maambukizi ya magonjwa hatari vitumike pale inapobidi kumshika mnyama au binadamu anayehisiwa kuathirika na HBU. Tahadhari hii inahusisha pia wale wote wanahusika na uchukuaji na usafirishaji wa sampuli zitokanazo na wagonjwa/wanyama wanaoshukiwa kuwa na maambukizi ya HBU

Taarifa hii imeandaliwa na:

**Calvin Sindato, Clement Mweya, Sharadhuli Kimera, Leonard Mboera**  
*Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Dar es Salaam, Tanzania*  
*Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Morogoro, Tanzania*

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:

Mkurugenzi Mkuu  
 Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu  
 3 Barabara ya Barack Obama  
 11101 Dar es Salaam, Tanzania  
 Simu: +255 222121400